TOLEO MAALUMU Na. 019 | APRILI 2025 | HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

Jarida la

# SAUTI YA JIJI

*Kazi Iendelee!*



# MIAKA MINNE YA RAIS DKT. SAMIA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

Scan kusoma jarida kidijitali

# MIAKA MINNE YA UONGOZI WA

## MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

*Jiji la Dar es Salaam Kazi Inaendelea!*



MHARIRI MKUU
**TABU FAITH SHAIBU**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

WAHARIRI WASAIDIZI
**GASTON MAKWEMBE**
Afisa Habari Mwandamizi

WAANDISHI
**SHALUA MPANDA**
Afisa Habari

**HASHIMU JUMBE**
Afisa Habari

**DOINA MWAMBAGI**
Afisa Habari

**PETER MABERE**
Afisa Habari

WAPIGA PICHA
**METHEW JONAS**
Afisa Habari

**RODNEY MALONGO**
Afisa Habari

MSANIFU WA JARIDA
**MICHOLAX MUSSA**
Afisa Habari



# Miaka 4 ya rais samia madarakani, jiji la DSM lajivunia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mafanikio

*Na **Hashim Jumbe***

Miaka Minne imepita tangu Taifa letu lilipoandika historia mpya ya kuwa na Amiri Jeshi Mkuu wa kwanza Mwanamke, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni mengi yameandikwa na mengi yameelezwa juu ya uwezo wake mkubwa wa kiuongozi katika awamu hii ya Sita (6).

Hotuba yake ya kwanza ya tarehe 22 Aprili, 2021 kwa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, ilitosha kutoa dira ya uongozi wake na Tanzania aitakayo, hivyo katika kipindi cha miaka minne (4) ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan teyari amefanya mapinduzi makubwa katika sekta ya afya, elimu, maendeleo ya jamii na sekta nyengine za uzalishaji mali ikiwa ni pamoja na masuala ya biashara.

Kwa upande wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kama ilivyo Halmashauri nyengine, jukumu lake kubwa la kwanza na la kisheria ni kuhakikisha kwamba inatoa huduma zilizo bora na endelevu kwa wananchi wake katika sekta za msingi, hivyo ni dhahiri sasa mafanikio yameanza kuonekana kwa kila sekta, kwani Serikali anayoiongoza Rais Samia, imefanikiwa kutimiza ahadi zilizoahidiwa kwa wananchi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025)

“Dhamira yetu ni kuhakikisha tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kwakweli kuhakikisha kwamba maendeleo ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam yanaonekana na yanaonekana dhahiri” alisema Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Ndugu Elihuruma Mabelya



# "Rais Samia ameongeza fedha kwenye Miradi ya Maendeleo" Mkurugenzi Mabelya

> **"Tunamshukuru Rais Samia kwa kutupatia zaidi ya Bilioni 300 kwa ajili Miradi ya Maendeleo"**

*Na* ***Shalua Mpanda***

Imekua ni miaka minne (4) yenye matokeo chanya kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, bajeti ya Halmashauri imekua ikiongezeka kila mwaka, hiyo imechagizwa na Rais Samia kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za afya, elimu na maeneo mengine muhimu.

"Katika kuhakikisha kwamba Ilani ya Uchaguzi inatekelezwa ipasavyo, maendeleo kwenye sekta muhimu tumeyazingatia, kwa miaka minne tumeona mabadiliko makubwa na nguvu ambayo Halmashauri imeweka, lakini pia Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amewekeza" alisema Mkurugenzi Mabelya

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilipanga kukusanya

Shilingi Bilioni 202.4, mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kukusanya Shilingi Bilioni 208.5, mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kukusanya Shilingi Bilioni 255 na mwaka 2024/2025 imepanga kukusanya Shilingi Bilioni 280

"Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa miaka minne kumekua na ongezeko kubwa la ukusanyaji wa mapato na hivyo kupelekea utekelezaji wa miradi mbalimbali ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwenda kwa kasi lakini kwa uhakika kwamba fedha za utekelezaji wa miradi hiyo zipo" alisema Mkurugenzi Mabelya

Mabelya aliendelea kufafanua "Kwa mwaka huu tunaoendelea nao wa 2024/2025 hadi sasa tumefikia 83% ya makusanyo maana yake mpaka tutakapofika mwisho mwa mwaka tunatarajia tutakwenda mbali zaidi, kwa hiyo hii ni katika eneo la utekelezaji wa mpango na bajeti ya Halmashauri yetu kwa kipindi cha hii miaka minne, inaonesha kuna ongezeko kubwa na sehemu kubwa ya ongezeko hili imekua ni kwa ajili ya kwenda kutatua kero zilizopo kwa wananchi wetu katika maeneo ya miundombinu ya utoaji wa huduma za msingi, hivyo tuna jukumu la kumshukuru Rais Samia"


Aidha, Mkurugenzi Mabelya alimalizia kwa kusema "Sisi Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tumejipanga vyema kuhakikisha tunakua na miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inafadhiliwa na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kama nilivyosema uwezo wa kukusanya ni mkubwa na hivyo tumejikita na kujielekeza katika kuhakikisha tunakua na miradi ya kielelezo au miradi ya kimkakati ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam"

> **"Miaka minne ya Serikali ya awamu ya sita imekuwa yenye matokeo chanya kwa Halmashauri ya Jiji letu."**
>
> **Ndg. Elihuruma Mabelya**
> Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam














# Wana-Ilala tunamshukuru Rais Samia ametoa Bilioni 28 kukarabati na kujenga soko jipya la kisasa Kariakoo - DC Mpogolo

*Na* ***Peter Mabere***

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, wananchi wa Ilala na wafanyabiashara wa Jiji la Dar es Salaam wameshuhudia mageuzi makubwa ya kiuchumi kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa soko la kisasa la Kariakoo, lililojengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 28 zilizotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Soko la zamani la Kariakoo liliteketea kwa moto mwaka 2021, na kuwaacha mamia ya wafanyabiashara bila eneo la kufanyia shughuli zao za kila siku. Tukio hilo liliathiri kwa kiasi kikubwa mzunguko wa biashara si tu kwa Kariakoo, bali pia kwa Jiji zima la Dar es Salaam. Kupitia uongozi makini wa Rais Samia, Serikali iliamua kujenga soko jipya la kisasa, linalozingatia viwango vya juu vya ubora, usalama, na heshima ya mfanyabiashara wa Kitanzania.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Mhe. Edward Mpogolo, amesema kuwa soko hilo sasa limekuwa alama ya matumaini na mafanikio kwa wananchi waliokuwa wameathirika moja kwa moja.

"Mhe. Rais Dkt. Samia ameonesha kwa vitendo namna anavyowajali wafanyabiashara wa Kariakoo na wananchi wa Ilala kwa ujumla. Serikali imetoa bilioni 28 kwa ajili ya kujenga soko hili kisasa, hatua ambayo inatoa fursa mpya kwa uchumi wa jiji letu," alisema Mhe. Mpogolo.

Soko hilo lina sehemu bora za biashara, njia pana kwa ajili ya wateja, maeneo ya kuhifadhia bidhaa, pamoja









na miundombinu rafiki kwa watu wote, wakiwemo wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu. Vifaa vya kisasa vimewekwa kuhakikisha huduma bora, zenye ufanisi na usalama.

Mheshimiwa Mpogolo pia amesisitiza umuhimu wa usafi wa soko hilo, akieleza kuwa usimamizi madhubuti utawekwa kuhakikisha mazingira hayo yanatunzwa kwa viwango vya juu.

"Usafi ni jukumu la kila mmoja wetu. Tutahakikisha kuwa mazingira haya yanatunzwa kwa kiwango cha juu, kwani soko hili lina hadhi ya kimataifa na linahitaji kuhifadhiwa kwa viwango vinavyolingana na uwekezaji uliofanyika," alisema.

Kuhusu ulinzi na usalama, Mhe. Mpogolo amesema kuwa soko hilo limewekewa taa za kisasa na kamera za usalama (CCTV) ili kuhakikisha kila shughuli inayofanyika inakuwa chini ya uangalizi, na kuwafanya wafanyabiashara na wateja kuhisi utulivu na usalama wakati wote.

Akihitimisha, Mhe. Mpogolo alisema: "Tuna kila sababu ya kumshukuru Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kusikia kilio cha wafanyabiashara wetu na kulifanyia kazi kwa kasi, ubora na umakini. Soko hili ni alama ya upya wa Kariakoo, na ni sehemu ya historia mpya ya mafanikio ya wananchi wa Ilala.



# Uimara wa Baraza la Madiwani chachu ya maendeleo ya jiji la Dar es salaam

*Na **Doina Mwambagi***

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Tanzania imeendelea kushuhudia mageuzi makubwa ya kijamii na kiuchumi. Kupitia dhamira ya kweli ya kuwaletea wananchi maendeleo ya kweli na huduma bora, Rais Samia ameweka msisitizo mkubwa katika kuimarisha miundombinu, kuboresha huduma za kijamii, na kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Jiji la Dar es Salaam limekuwa miongoni mwa maeneo yaliyonufaika zaidi na juhudi hizi. Hili limewezekana kwa sababu ya uimara wa Baraza la Madiwani wa Jiji ambao wamekuwa chachu ya utekelezaji wa dira ya maendeleo ya Mheshimiwa Rais kwa bidii, mshikamano na usimamizi makini wa rasilimali.

Mojawapo ya sababu zilizochangia mafanikio ya Jiji la Dar es Salaam ni ushirikiano thabiti uliopo kati ya Baraza la Madiwani na watendaji wa Halmashauri. Madiwani wamekuwa wakitoa maelekezo ya kimkakati yanayotokana na mahitaji halisi ya wananchi, huku watumishi wakitekeleza kwa weledi na ufanisi.

Katika kila mwaka wa fedha, Baraza la Madiwani limekuwa mstari wa mbele kushiri-

ki kikamilifu kwenye mchakato wa kupanga, kujadili na hatimaye kupitisha bajeti ya Halmashauri. Ushirikiano huu umehakikisha kuwa bajeti inazingatia vipaumbele vya wananchi na kwamba utekelezaji wake unasimamiwa kwa karibu. Kupitishwa kwa bajeti kwa Baraza la Madiwani limekuwa pia mstari wa mbele kuhakikisha utoaji wa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu unatekelezwa kwa ufanisi. Mikopo hii imechangia kuinua vipato vya wananchi na kuwafanya fanikisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo, sambamba na dhamira ya Mheshimiwa Rais Samia ya kuwaletea wananchi maisha bora na huduma zenye tija."

Miaka minne ya Rais Samia Suluhu Hassan imeonyesha





wakati kumechangia utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa ufanisi na kuondoa ucheleweshaji wa huduma muhimu kwa jamii.

Kupitia usimamizi wa pamoja kati ya madiwani na watendaji, miradi mingi ya maendeleo imetekelezwa. Hii ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa barabara, shule, na vituo vya afya katika maeneo mbalimbali ya jiji. Maboresho haya yamechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto za usafiri, kuongeza upatikanaji wa elimu, na kuimarisha huduma za afya kwa wananchi.

washiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi. Wananchi wengi waliokuwa hawana mitaji sasa wameweza kuanzisha biashara ndogo ndogo, vikundi vya uzalishaji, na miradi ya ujasiriamali inayowasaidia kujitegemea.

Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Mhe. Omary Kumbilamoto, amepongeza kazi kubwa iliyofanywa na Baraza la Madiwani kwa kushirikiana na watendaji wa Halmashauri, amesema "Baraza letu limekuwa imara na linafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa. Hii ndiyo siri ya mafanikio tunayoyaona leo. Kwa pamoja, tume- wazi kuwa maendeleo ni matokeo ya mshikamano, maono ya pamoja na utendaji wenye kuwajali wananchi. Uimara wa Baraza la Madiwani wa Jiji la Dar es Salaam, kwa kushirikiana na watumishi wa Halmashauri, umeendelea kuwa mfano wa uongozi bora unaochochea maendeleo na kuboresha maisha ya wananchi wa kawaida. Kama ambavyo Rais Samia amesisitiza mara kadhaa, maendeleo ya kweli ni yale yanayoonekana katika maisha ya wananchi kauli ambayo halmashauri ya jiji Dar es Salaam inatekelezwa kwa vitendo.




# Rais Samia ameshusha neema sekta ya elimu katika Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam

*Na* ***Shalua Mpanda***

Ndani ya miaka minne ya Uongozi wa Rais Samia, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeshuhudia maboresho makubwa katika sekta ya elimu kulingana na azma yake ya kuhakikisha elimu inakuwa ni kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa kutoa wahitimu wenye ujuzi na stadi.

***i. Elimu ya Awali na Msingi***

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Samia, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi, imeweza kupokea fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za walimu, ujenzi wa ofisi za walimu, ujenzi wa shule mpya pamoja na utengenezaji wa madawati na vifaa vya kujifunzia na kufundishia kutoka Serikali Kuu, wafadhili wa elimu na mapato ya ndani ya Halmashauri.

"Tumepokea zaidi ya Shilingi Bilioni 20.5 katika kipindi cha miaka minne, fedha hizi zimetoka Serikali Kuu, wafadhili pamoja na mapato ya ndani, kwa hiyo tunamshukuru sana Mhe. Rais kwa

kutuwezesha kupata fedha zote hizi ambazo zimetuwezesha kujenga vyumba vya madarasa 437 ambavyo wanafunzi wemeweza kuingia na kupata huduma ya kusoma kirahisi" Mwl. Magreth Macha, Afisa Elimu Awali na Msingi, Jiji la Dar es Salaam.

"Lakini pia Halmashauri yetu ya Jiji la Dar es Salaam kupitia mapato yake ya ndani tumeweza kutengeneza madawati 31,539 ambayo yana thamani ya Shilingi Bilioni 3.9 ambayo tumeyasambaza katika shule zetu zote zile ambazo zina upungufu wa madawati" aliongeza Mwl. Macha



*Picha ya majengo ya shule mpya ya Sekondari Gunatra iliyopo kata ya Msongola, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.*

"Halkadhalika kwa kipindi hiki cha miaka minne tumeweza kupata fedha ya ruzuku ya uendeshaji kiasi cha Shilingi Bilioni 7.8 kwa ajili ya posho ya madaraka, chakula cha wanafunzi wenye mahitaji maalumu, fedha ya uendeshaji utawala, ununuzi wa vifaa, mitihani na shughuli za michezo" alisema Mwl. Macha

Aidha, katika kipindi hiki cha miaka minne Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweza kujenga shule mpya kumi na mbili (12) zenye jumla ya Shilingi Bilioni 3.3 kwa hiyo kwa kipindi hiki cha miaka minne Halmashauri imekua na mafanikio makubwa sana, shule hizi zimejengwa kupitia mapato ya ndani, lakini na fedha kutoka Serikali Kuu, fedha zilizotoka Serikali Kuu ni kwa ajili ya miradi mitatu (03) ya BOOST, LENS na EP4R

Kupitia mradi wa kuboresha elimu ya awali na msingi (BOOST) Serikali imejenga shule mpya nne (04) ambazo ni Shule ya Msingi Mshikamano, Kifuru Mpya, Mnyamani na Mzizima, kwaajili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na miundombinu "Lakini pia tunazo shule

nyengine ambazo tumejenga, nazo ni Zogoali, Nguvu mpya, Mizengo Pinda, Guluka kwalala, Taliani, Kipera na Mwembe ambazo zimejengwa kwa fedha za mapato ya ndani na zimesaidia wanafunzi kwenda shule kwa urahisi na hizi ni huduma ambazo tumezisogeza kwa wananchi ili wananchi waweze kupata huduma kwa urahisi, watoto wao wasitembee mbali" alisema Mwl. Macha

Kwa upande wa ukarabati wa vyumba vya madarasa, Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani imepeleka fedha za kutosha kwenye shule mbalimbali "tumepeleka Shilingi Milioni 540 za mapato ya ndani, tumeweza kukarabati shule 36 ambapo tumepunguza changamoto ambazo zipo kwenye mashule, lakini bado tunaendelea kupeleka fedha" alimalizia Mwl. Macha

Sambamba na hayo lakini pia kwa kipindi cha miaka minne, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweza kujenga majengo (7) ya utawala yenye thamani ya Shilingi Milioni 297.6, matundu ya vyoo 1,063 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.01, ujenzi wa mabweni (2) kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, thamani yake ni Shilingi 177.6 na shule (3) zinazoendelea kujengwa zenye thamani ya Shilingi Milioni 509.6 shule hizi ni Chakenge, Mvuleni na Shule ya Bangulo Anex

### *ii. Elimu ya Sekondari*

Katika kipindi cha miaka minne, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imepokea jumla ya Shilingi Bilioni 35.5 katika Idara ya Elimu Sekondari, ambazo Tshs. Bilioni 11.3 zimetoka Serikali Kuu na kujenga vyumba vya maadarasa 255 katika awamu ya kwanza maarufu kama fedha ya UVIKO 19 na vyumba vya madarasa 310 kwa awamu ya pili kwa maana Pochi ya Mama

"Pamoja na hayo, tumekuwa na mradi wa kuboresha elimu ya sekondari (SEQUIP) ambapo Serikali imetoa fedha kwa Halmashauri ili kuwezesha upatikanaji wa elimu, ikiwa ni pamoja na mazingira salama ya wasichana kupata elimu, kupitia mradi huo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweza kujenga Shule ya Sekondari Liwiti, Gunatra na sasa ujenzi wa Shule Mpya ya Ghorofa Kitunda Relini" alisema Mwl. Mussa Ally, Afisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

Kwa upande wa mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, jumla ya fedha Shilingi Bilioni 15.5 zimeweza kutumika kujenga miundombinu ya madarasa, vyoo, kumalizia maabara, kujenga majengo hasa madarasa ya ghorofa "kwa sasa tunaendelea na ujenzi wa maghorofa nane (08) katika shule za sekondari za Mnazi Mmoja, Minazi Mirefu, Kipunguni, Kimanga, Shule mpya ya Amani, Ilala Kasulu, Msimbazi na Liwiti, ambapo ghorofa moja lina uwezo wa kubeba madarasa 20 na matundu ya vyoo 45" alisema Mwl. Mussa Ally

Katika kutekeleza Ilani ya CCM sura ya 3 ibara ya 80 (a-q) kwenye kuongeza fursa, ubora na manufaa kwa wakaazi, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imehakikisha kwamba maeneo yote ambayo hayakua na shule, yanakua na shule, mfano Kata ya Liwiti utakuta kuna shule kubwa ya kisasa ambapo mpaka miundombinu itakapokamilika tutakuwa tumetumia jumla ya fedha Tshs. Bilioni 3.5, kwa sasa jengo limegharimu Tshs. Bilioni 1.8 lenye madarasa 20, matundu ya vyoo 45 pamoja na sehemu ya lift limekamilika, kadhalika majengo yatakayofuata ni ambayo yatabeba maabara na miundombinu mingine kama vile ukumbi na jengo la utawala" aliongeza Mwl. Mussa Ally



*Picha ya majengo ya shule mpya ya Sekondari Amani iliyojengwa kataya Ukonga.*

Aidha, kwa upande wa elimu bila malipo, Serikali ya awamu ya Sita imeendelea kutoka fedha kwa ajili ya kugharamia upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi "Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka minne tumepokea fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 12.2 fedha zinazokuja kwa ajili ya kulipa elimu bila malipo kwa maana ya kusaidia watoto shuleni" alisema Mwl. Mussa

"Kwa upande wa vitabu, tumekuwa tukipokea kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania na mapato ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ili kuhakikisha wanafunzi wanapata vitabu vya kiada na ziada, jumla ya fedha Shilingi Milioni 216.2 zimetumika kununua vitabu vya kiada" alisema Mwl. Mussa

Ili kuhakikisha kila mtoto anasoma akiwa ameketi, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, na hili ni agizo la Serikali chini ya usimamizi wa Dkt. Samia, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kwamba watoto wote wanasoma wakiwa wameketi, Halmashauri imeweza kutengeneza viti na meza

"kwa idara ya elimu sekondari pekee kwa mwaka 2023/2024 tumetengeneza viti na meza 17,500 na mgawanyo sawia umefanyika kwenye shule zetu ili watoto waweze kuketi. Madawati hayo yamegharimu jumla ya fedha Shilingi Bilioni 1.4" alimalizia kwa kusema Mwl. Mussa




*Picha ya mabwebi ya Wanafunzi wa kike katika shule ya Sekondari Mvuti.*



# Rais Samia amefanya miujiza mikubwa Sekta ya Afya

*Na **Doina Mwambagi***

Tangu alipoingia madarakani, Rais Samia ameonesha miujiza mikubwa katika sekta ya afya kwa kuzingatia kuwa afya ni zaidi ya rasilimali muhimu kwenye maisha ya kila mmoja wetu na ustawi wa Taifa, hivyo Rais Samia ameendelea kufanya jitihada mbalimbali ili kupambana na adui maradhi.

"Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kila unapojaribu kuongelea bado hujapata mfano wake wa kumuongelea, kwa kipindi cha miaka minne hii Jiji la Dar es Salaam imekua ni faraja na furaha kubwa sana, Idara ya Afya imepokea kiasi cha fedha Shilingi Bilioni 101.4 kutoka Mapato ya ndani ya Halmashauri, Serikali Kuu na Wafadhili kwa ajili ya ujenzi wa vituo vipya vya afya, zahanati na hospitali pamoja na ununuzi wa dawa na vifaa tiba" alisema Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dkt. Zaitun Hamza

Kupitia mapato yake ya ndani, Idara ya Afya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka minne imepata kiasi cha Shilingi Bilioni 35.4 ikiwa ni pamoja fedha za ujenzi wa Hospitali (3) za kila Jimbo.

Aidha, kwa fedha za Serikali Kuu, Idara ya Afya imetekeleza miradi mbalimbali,

ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 5.2 kimegharamia ujenzi wa vituo vya afya vinne ambavyo ni Segerea, Mchikichini, Guluka Kwalala na Kipunguni 'B' lakini pia ujenzi wa wodi 3, majengo manne ya upasuaji, wodi ya upasuaji wanawake na wanaume na jengo la kuhifadhia maiti, ujenzi mwengine ni wa jengo la dharura, ujenzi wa vyumba vya kujifungulia akina Mama Gongolamboto, Bangulo, Zahanati ya Nzasa na Luhanga.

"Mhe. Rais yeye ametimiza wajibu wake, kile kipande ambacho Mwenyezi Mungu amemkatia katika hii Dunia ambapo ni Tanzania kuhakikisha analeta faraja na matumaini kwa watanzania kuwapelekea huduma za afya karibu na wananchi wake waweze kupata muda mchache wa kupata huduma na waweze kuendelea na shughuli zao za maendeleo" alieleza Dkt. Zaituni Hamza

Lakini pia Idara ya Afya imetumia kiasi cha Shilingi Bilioni 17.5 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa vituo vya afya ambavyo ni Mzinga, Mchikichini, Kiwalani, Kinyerezi, Zingiziwa na Majohe, ujenzi wa jengo la macho na meno Kivule, jengo la bima na kuongeza ghorofa moja kituo cha mnazi mmoja.

Haijaishia hapo, huwezi kujenga tu bila ya kuweka dawa na vifaa tiba, katika kipindi cha miaka minne ya Uongozi wa Rais Samia, ameweza kutoa fedha zaidi ya Shilingi Bilioni 42.9 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba "haijawahi kutokea, ndani ya hii miaka minne, fedha zimekua zikishushwa ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwa hiyo ni kitu kikubwa sana cha kujivunia kwa maana kwamba hakujenga tu, lakini dawa na vifaa tiba vimeletwa" Dkt. Zaituni Hamza

"Kama mlivyoona katika program ya mama ya 'M-Mama' sasa tunakwenda kuboresha mfumo mzima wa 'referral system' kwa ajili ya kumuokoa mama na mtoto wake, kwa maana kwamba kupata ujauzito siyo sababu ya mama kwenda kufariki, kwa hiyo kuna mafanikio makubwa sana" alifafanua Dkt. Zaituni Hamza

Kwenye eneo la uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma, Rais Samia ameimarisha miundombinu ya kutolea huduma za dharura kwenye Hospitali ya EMD iliyopo Ukonga Magereza "Mhe. Rais ametuletea vifaa kwa ajili ya huduma za dharura kwenye hospitali ya EMD ambayo ipo Ukonga Magereza, kwa hiyo ukiangalia kwenye kuboresha huduma Mhe. Rais amejitahidi sana kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam" Dkt. Zaituni

Halkadhalika, Serikali pia imewekeza kwa kiwango kikubwa katika eneo la huduma za uchunguzi ambapo imeshajenga jengo la x-ray kituo cha afya cha Pugu "Uwekezaji huu umewezesha upatikanaji wa huduma za uchunguzi karibu zaidi na wananchi ambapo hapo awali huduma za uchunguzi. zilikuwa zinapatikana katika Hospitali kama vile Amana na Mnazi Mmoja, hivyo kuwalazimu wagonjwa kutumia gharama kubwa kufuata huduma" Dkt. Zaituni








# Jiji la dar es salaam lavunja rekodi katika nishati safi kwa kulinda mazingira na afya za wananchi


Na ***Doina Mwambagi***

Katika kipindi cha miaka minne (4) ya Uongozi wa Rais Samia, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imewajengea mazingira mazuri wananchi kupata mikopo nafuu isiyo na riba ambayo imeleta tija katika ukuaji wa uchumi kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

"Kupitia mfuko wa 10% ya mapato ya ndani, kwa kipindi cha miaka minne (4) Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweza kutoa kiasi cha Shilingi Bilioni 23.5 kwa vikundi 1,465 vyeny e wanufaika 9,399 ambapo vikundi vya wanawake ni 865 vyenye wanufaika 6,075 vijana ni 428 wanufaika 2,875 na wenye ulemavu ni 172 wanufaika 452" Francisca Makoye, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Itakumbukwa kua Aprili, 2023 Serikali ilitoa agizo la kusimamisha utoaji wa mikopo ili kujipa muda wa kufanya maboresho ya kanuni na mwongozo wa utoaji na usimamizi wa mikopo hii. Katika utaratibu ulioboreshwa, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ni miongoni mwa Halmashauri (10) za mfano katika kutoa mikopo kwa kutumia mfumo jumuishi

"Mpaka sasa kiasi cha Shilingi Bilioni 15.3 kimetengwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwaajili ya kukopeshwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu mara baada ya mfumo jumuishi ambapo Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam itatoa mikopo hii kwa kushirikiana na Benki ya CRDB na Benki ya NMB. Hadi Februari, 2025 jumla ya vikundi 945 vimepokelewa katika mfumo wa WEZESHA na vipo hatua mbalimbali za mchakato wa kupata mkopo." alisema Makoye



**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**
S.L.P 20950
1 BARABARA YA MOROGORO
11882 DAR ES SALAAM
**SIMU:** 0738 378 386
**NUKUSHI:** 2128800
**BARUA PEPE:** info@dcc.go.tz
**TOVUTI:** www.dcc.ho.tz